4. Watu fulani katika kundi walisema nini wakati Pilato aliwatolea Yahshua ili wapate kumhukumu wao wenyewe? Yohana 18:31; Yohana 19:7.
5. Yahshua alikufa saa ngapi ? Mathayo 27:45, 46, 50
6. Ni wakati gani wa siku mwili wake uliwekwa kaburini? Mathayo 27:57-60.
7. Je, ni nini maana ya neno"jioni" katika Bibilia? Kumbukumbu la Torati 16:6; 2 Nyakati 18:34; Marko 1:32.
8. Danieli alisema nini kitatokea Yerusalemu kufuatia kusulubiwa kwa Yahshua Masihi? Danieli 9:26.

   Maelezo: Ni kweli unaojulikana katika historia kwamba Tito jemedari wa Kirumi aliizingira Yerusalemu kutoka 66-70A.D na mji pamoja na hekalu zikaharibiwa.

9. Mwokozi wetu mpendwa alitupa mfano wakujitoa dhabihu na hata kifo katika kuwaokoa wengine kwa ajili ya ufalme. Tumeamrishwa kujitoa dhabihu yoyote ya maisha yetu na rasilimali zetu ili kusaidia kuwaokoa wengine? Warumi 12:1.

******************************



nao vipi na kwa nini? Kumbukumbu la Torati 7: 5-6.

6. Chini ya agano jipya au mafundisho ya agano, Elohim amewaita, na bado anaita watu kwa ajili ya Jina Lake. Je! Tunapaswa kuuchukuliaje ulimwengu, au wale ambao hawamo katika Masihi? Waefeso 5: 1-7.
7. Je! Hii inalingana na maneno ya Yahshua? Mathayo 5: 21-26, 38-48.
8. Funzo nzuri la kutenganisha mvuto, mema na mabaya, litapatikana katika 2 Wakorintho 6: 14-16. Je! Tunapaswa kufanya nini juu yake? 2 Wakorintho 6: 17-18.
9. Je! Unaelewa nini kwa kuwa katika ulimwenguni lakini sio wa ulimwengu? Yohana 17: 6, 11,12,15,16.

******************************

**Somo la Januari 23, 2021 (Shevat 10, 5781).**

## IMANI NA KUTII

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 10: 1-14.**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 11: 6.**

1. Je! Yahshua alisema nini kuhusu imani? Marko 9:23.
2. Je! Paulo alisema nini kuhusu wale waliokufia jangwani? Waebrania 3:16, 17.



9. Ni matendo gani yanaashiria kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Masihi? Warumi 6:3-6.
10. Jinsi gani Masihi alijidhihirisha kwa Yohana katika kisiwa cha Patimo? Ufunuo 1:17, 18.

******************************



***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡

# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Kwanza
2021

Ya
Januari, Februari, Machi.
**(Tevet, Shevat, Adar, Nisan)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡✡

3. Ni kwa nini hawangeweza kuingia kwenye Nchi ya Ahadi? Waebrania 3:19.
4. Kwa kutazama tukio lao, tunashauriwa vipi? Waebrania 4: 1, 2.
5. Jinsi gani wana wa Israeli walionyesha kutokuamini kwao? Ezekieli 20:15, 16.
6. Je! Ni nini hufuata imani ya kweli kila wakati? Yakobo 2:18.
7. Ni kwa nini mapungufu ya watu wa zamani yameandikwa ili tusome? 1 Wakorintho 10:11.
8. Je! Elohim alimwamuru Sauli afanye nini? 1 Samweli 15: 1-3.
9. Alitimizaje maagizo haya? 1 Samweli 15: 7-9.
10. Sauli alimsalimiaje Samweli? Mazungumzo yao yalikuwa gani? 1 Samweli 15: 13-21.
11. Jinsi gani Samweli aliyajumulisha haya? 1 Samweli 15:22, 23.
12. Je! Ni nini ilikuwa sababu ya kifo cha mapema cha Sauli? 1 Mambo ya Nyakati 10:13, 14.
13. Je! Paulo anatuhimiza tuzingatie neno la Bwana aje? Waebrania 2: 1-3.
14. Je! Ghadhabu ya Elohim itakuwa juu ya wasiotii? Waefeso 5: 6; Wakolosai 3: 6.

**Maelezo**: Imani, (kuamini kwa kweli), ni kutii. Na ikiwa hatutatii, basi hatujapata kusikia kweli. Warumi 10:17; Waebrania 5: 9.

*******************************



7. Ni mambo gani ya aibu ambayo yalifanywa kwake katika nyumba ya kuhani mkuu? Luka 22: 62-64.
8. Ni ukatili gani Pilato alimfanyia? Yohana 19.
9. Ni mambo gani ya aibu aliyopokea kutoka kwa askari? Mat. 27:29, 30, 34, 41, 42.
10. Je! Ni maombi gani mazuri aliyoyatoa kwa watesi wake wakati akiwa ametundikwa msalabani? Luka 23:34.
11. Je! Ilikuwa muhimu Masihi atesewe hivi? Ebr. 2:10.
12. Kuona jinsi Masihi aliruhusiwa kuteseka hivi vyote kwa ajili yetu, mateso haya ni changamoto gani kwa wafuasi Wake? Warumi 8:31, 32.

*******************************

### Somo La Machi 6, 2021 (Adar 22, 5781).

## KUSULUBIWA KWA MASIHI

**Somo Kuu: Mathayo 27: 11-37.**
**Fungu La Kukariri: Isaya 53: 8.**

1. Paulo alisema nini kuhusu kifo na ufufuo wa Yahshua? 1 Wakorintho 15:3, 4.
2. Yahshua aliwaambia wanafunzi wake kwamba Atasulubiwa? Mathayo 16:21; 17:22, 23
3. Ni watu gani ambao walimhukumu Bwana Yahshua? Marko 10:32-34.



### Somo la Januari 2, 2021 (Tevet 18, 5781).

## KIZAZI NA KUZALIWA KWA YAHSHUA

**Somo Kuu: Mathayo 1.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 1:23.**

1. Je! Mwanzo wa Mathayo umepangwaje? Je! Yahshua anasemekana ni mwana wa nani? Mathayo 1: 1.
2. Je, Luka anasema nini juu ya hili? Luka 1: 30-33.
3. Ni nani alikuwa wa mwisho katika kizazi cha Masihi kutajwa? Mathayo 1:16.
4. Kuna vizazi vingapi kutoka kwa Ibrahimu hadi Daudi; kutoka Daudi hadi utumwani Babeli, na kutoka huko hadi Masihi? Mstari wa 17.
5. Je! Kulikuwa na uhusiano gani kati ya Yusufu na Mariamu kabla ya kuzaliwa kwa Yahshua? Mstari wa 18.
6. Tabia ya Yusufu ilikuwa gani? Alikusudia kufanya nini kwenye hafla hii? Mstari wa 19.
7. Alizuiliwaje kutekeleza mpango wake? Alihakikishiwa nini? Mstari wa 20.
8. Je! Malaika alisema Mariamu atamzaa nani? Mstari wa 21.
9. Je! Hii yote ilikuwa kulingana na nini? Mstari wa 22.



### Somo La Machi 27, 2021 (Nisan 14, 5781).

## MAANA YA KIFO NA KUFUFUKA KWAKE YAHSHUA KWETU SISI

**Somo Kuu: 1 Wakorintho 15:1-23**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 15:22, 23.**

1. Je, ni sababu gani Isaya alitoa kwa ajili ya unabii wa kifo cha Masihi? Isaya 53: 8.
2. Je, Kifo cha Masihi Mwana, kiliamriwa na Elohim Baba? Isaya 53: 6, 10.
3. Je, mwana wa Elohim alijitolea, au alilazimishwa kufa? Mathayo 26:53; Yohana 10:17, 18.
4. Je, Masihi alitabiri kifo na kufufuka kwake mwenyewe? Mathayo 20:18, 19, 16:21-23.
5. Je, baadaye Masihi alikuwa nani? Waebrania 5:8, 9.
6. Jinsi gani tunafaa kukumbuka kifo cha Yahshua? 1 Wakorintho 11:26-32.
7. Yahshua alitabiri nini kuhusu kufufuka kwake? Yohana 2:19-22; Marko 9:31.
8. Kwa nini maisha, kifo na kufufuka kwa Masihi Yahshua, mwana wa Elohim, kulikuwa kwa muhimu? (a) ili kutimiza maandiko: Luka 24:44-46; (b) kwa ajili ya msamaha wa dhambi:1 Wakorintho 15:17; (c) kwa ajili ya kuhesabiwa haki: Warumi 4:25; (d) ili kufanya maombezi: Warumi 8:34; Waebrania 9:24.

alipenda hadi mwisho. Hakuweza ndani Yake kuwachukia waliomuua. Katika saa Yake ya uchungu mwingi alimwomba Elohim awasamehe. Funzo lake katika upendo; Mfano wake wa kujitoa dhabihu, hauwezi kuthaminiwa kabisa.

**Somo Kuu: Isaya 53: 1-12.**
**Fungu La Kukariri: I Timotheo 1:15.**

1. Ni kwa nini Masihi alikuja ulimwenguni? 1 Tim. 1:15.
2. Ni nini kilichomfanya Elohim kumruhusu Mwanawe mpendwa afe kwa ajili ya watu wenye dhambi? 1 Yohana 4: 9-10; Warumi 5: 8.
3. Je! Masihi alijua mapema jinsi atakavyochukiwa na kudharauliwa, na mwishowe asulubiwe? Luka 18: 31-33.
4. Yahshua alijua yote yatakayompata, na jinsi atakavyoteseka na kusulubiwa. Alikuwa tayari kwa kiasi gani kupitia uchungu huu wote, aibu, na mateso? Luka 22: 41-42; Mat. 16: 21-23; 26: 37-39.
5. Je uchungu wa roho Yake ulikuwa mkubwa kiasi gani na ni nini kilichotokea na kumsababishia huzuni zaidi? Luka 22:44, 47, 48.
6. Ni kitendo gani cha Petro kilichosababisha Mwokozi mateso zaidi? Luka 22: 59-61.



**Somo La Januari 30, 2021(Shevat 17, 5781).**

## IMANI KATIKA NENO LA ELOHIM

**Somo Kuu: Warumi 4**
**Fungu La Kukariri: Warumi 4:3**

1. Taja mambo manne imani ilitimiza katika Waebrania 11:2-5.
2. Ni nini Nuhu aliweza kutimiza kwa imani? Ni urithi gani wa kiroho ulikuwa wake kutokana na tendo hili? Waebrania 11:7.

   **Maelezo**: Kwetu tendo hili laweza kuonekana rahisi. Lakini watu wa siku hizo hawakua wameona mvua mbeleeni, na kwa kawaida hawangeweza kuamini kwamba mvua itaiharibu dunia. Nuhu alimwamini Elohim bila ya kujali jinsi jambo hilo lingewezekana. Kwa hivyo lazima tuwe na imani sawa kama hiyo kwa Muumba wetu, kumwamini kikamilifu, kupitia uzoefu wetu wote wa maisha yetu ya sasa?

3. Ni kwa jinsi gani imani ya Abrahamu ina athiri mataifa ya ulimwengu? Warumi 4:11-13.
4. Kwa nini matukio ya Ibrahimu yaliandikwa? Warumi 4:23, 24.
5. Ni ahadi gani ya Elohim inatimizwa sasa katika tendo hili? Mwanzo 17:5-8.



hutuambia kwamba kikombe ambacho Yahshua alibariki kilikuwa na matunda ya mzabibu. Hii ilikuwa damu safi ya zabibu, ambayo inawakilisha damu ya thamani ya Yahshua. Tafadhali angalia Kumbukumbu 32:14, sehemu ya mwisho. Elewa kwamba kilichomo ndani ya kikombe hiki hakikuwa na divai iliyochachuka, wala maji, lakini ni damu ya zabibu, matunda ya mzabibu.

11. Je, ni sawa katika maandiko kwa kuita chakula cha jioni cha Bwana kama ushirika? 1 Wakor. 10:16.

    **Maelezo**. - Paulo akiandikia kanisa la Elohim huko Korintho kuhusu Chakula cha jioni cha Bwana ambacho Yahshua alianzisha wakati walipokuwa wakila Pasaka, kabla ya kuhukumiwa kwa ukatili alikiita Chakula cha jioni cha Bwana, au ushirika.

12. Je, Yuda alikuwapo na alishiriki katika chakula cha jioni cha Bwana? Luka 22:21; Yohana 13:18.
13. Je, kila mtu anapaswa kufanya nini kabla ya kula chakula cha jioni cha Bwana? Ikiwa tutashindwa, matokeo ya kusikitisha yatakuwa yapi? 1 Wakor. 11: 27-30.

******************************



10. Je! Isaya alitabiri nini juu ya hili? Mstari wa 23.
11. Je! Paulo anasema nini kuhusu utimilifu huu? 1Timotheo 3:16.
12. Je! Yusufu alikuwa na mtazamo gani baada ya ndoto hii? Mathayo 1:24.
13. Je! Mtoto Masihi alipewa jina gani? Mstari wa 25.
14. Umuhimu wa jina hili umesisitizwa vipi? Matendo 4: 10-12; Wafilipi 2: 9-11.

******************************

**Somo la Januari 9, 2021 (Tevet 25, 5781).**

## KUTAHIRIWA NA UBATIZO WA YAHSHUA MASIHI

**Somo Kuu: Yohana 1: 1-34.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 3:11.**

1. Wakati Yahshua alifikia umri wa siku nane, ni nini kilifanywa kulingana na sheria? Aliitwa jina gani? Luka 2:21; 1:31.

   **Maelezo**: Tunaona jinsi Yahshua na Yohana Mbatizaji walivyopewa majina na Malaika Gabrieli kabla ya kuzaliwa kwao. Pia fahamu kwamba katika visa vyote amri ya Mbinguni ilitiiwa.

6. Jinsi gani Mtume Paulo anatafsiri neno "uzao"? Wagalatia 3:16.
7. Kama Ibrahimu, jinsi gani tutakubali ahadi za Elohim? Warumi 4:21; Waebrania 11:6.
8. Imani ya kuokoa yafaa ijengwe kwa nini? Warumi 10:17.
9. Ikiwa tutasikia neno na kukosa kutenda kulingana na hilo neno, tumefananishwa na nini? Yakobo 1:22-24.
10. Ni siri gani katika kupokea baraka za Elohim, ambayo sisi sote tunapaswa kutamani katika utendaji wa kazi yetu katika dunia hii? Yakobo 1:25.

*******************************

**Somo la Februari 6, 2021 (Shevat 24, 5781).**

## TUNDALA ROHO

**Somo Kuu: Wagalatia 5: 14-26.**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 5:22, 23.**

1. Yahshua alisema nini kuhusu Ufalme wa Elohim? Luka 17:21 (sehemu ya mwisho). Angalia pambizo pia.
2. Je! Ni kwa uzoefu gani wa kiroho Ufalme wa Elohim unaanzishwa moyoni? Warumi 14:17.
3. Roho wa Elohim anakaa wapi? 1 Wakorintho 3:16; 6:19.



8. Je! Hii inajibu maombi ya Yahshua katika Yohana 17? Mstari wa 21-23.
9. Basi je, tunakuwa tayari kuwa watumishi wa maana kwa ajili yake? 2 Tim. 2: 19-21.
10. Ikiwa mtu hajatimiza mahitaji na kuwa mtakatifu, yeye ni nini? 2 Wakor. 13: 5; Tito 1:16.
11. Tukishatengwa kutokana na ulimwengu (kutakaswa), tutaupenda ulimwengu, na kutamani kuwa kama ulimwengu? 1 Yohana 2:15; Wakolosai 3: 1, 2; Warumi. 12: 2.
12. Tukishatembea na Elohim kama vile Enoku wa zamani, je! Tutazika talanta zetu katika vitu vya ulimwengu au tutazitumia kwa utukufu wa Baba wa Mbinguni kama watumishi wa faida katika shamba lake la mizabibu? Mathayo. 25:17, 18, 19, na mstari wa 30.

*******************************

**Somo la Februari 27, 2021 (Adar 15, 5781).**

## KUTESEKAKWA MASIHI

Mateso mabaya ya Bwana wetu Yahshua Masihi yameonyeshwa vizuri katika Maandiko ili tuweze kutambua kiwango cha dhamana aliyolipa kutuokoa kutoka kwa dhambi na mauti. Ni vigumu, hata hivyo, kutambua kiwango cha upendo ambao ulimlazimisha kufa badala yetu. Maandiko yanasema kwamba



2. Ni kwa sababu gani Yahshua aliletwa hekaluni? Luka 2: 22-24.
3. Wakati Simeoni alikuwa amemshika Yahshua mikononi mwake alitabiri nini? Luka 2:34.
4. Baada ya hii Yusufu na Mariamu walimpeleka wapi mtoto mchanga? Luka 2:39, 40.
5. Yusufu na Mariamu walikuwa waaminifu kiasi gani katika kutii Neno la Elohim kuhusu ibada? Luka 2:41. Linganisha na Kumbukumbu la Torati 16: 1, 16.
6. Ni nini kilitokea wakati mmoja walipokuwa Yerusalemu? Luka 2: 42-52.

**Maelezo**: Madaktari (wasomi) hawa walikuwa watumishi wa siku hiyo (Waandishi na Mafarisayo) sawa na watumishi wa siku hii na digrii zao za masomo. Katika Waebrania 1: 7 tunasoma "Na kwa habari za Malaika asema, Afanyaye malaika zake kuwa pepo, Na watumishi wake kuwa miali ya moto." Pia Zaburi 104: 4. Yahshua aliwachagua wanaume ambao ilisemekana walikuwa wajinga na hawajasoma. Hawakuwa na Shahada ya Sanaa au Daktari wa Shahada za Theologia, lakini walikuwa wanaume wenye nguvu za Elohim, wakijisalimisha kwake kikamilifu na kujazwa na Roho Mtakatifu wa Elohim. Tafadhali soma Isaya 56: 10-12.



5. Je,Wayahudi walilichukuliaje neno hili ambalo Yahshua alinena? Yohana 6:42.
6. Yahshua alijibu aje manung'unika yao? Yohana 6:48, 50, 51, 53-58.
7. Wakati Yahshua alianzisha chakula cha jioni cha Bwana, alisema mkate usiotiwa chachu uliashiria nini? Luka 22:19 Mat. 26:26. Linganisha na Yohana Mtakatifu 6:51, 53.

**Maelezo**. - Wakati Yahshua na wanafunzi wake walipokuwa wakila Pasaka, Yahshua alichukua mkate, akaubariki na akasema, chukua mle huu ni mwili wangu. Mkate huu usiochachwa uliwakilisha Mwili Wake. Kumla kondoo wa Pasaka sasa ilikuwa mambo yaliyokwisha milele. Pasaka ilikuwa historia. Yahshua alikuwa akianzisha Chakula cha jioni cha Bwana.

8. Baada ya kula mkate usiotiwa chachu, Yahshua alifanya nini? Luka 22:20; Mat. 26:27.
9. Je, Yahshua alisema kinywaji kilichokuwa katika kikombe kiliwakilishwa nini? Marko 14:24; Mat. 26:28; Luka 22:20. Linganisha na Yohana 6:53, 54.
10. Je, kikombe ambacho Yahshua aliwapa wanafunzi wake kilikuwa na nini? Marko 14:25; Mat. 26:29.

**Maelezo**. - Injili za Mtakatifu Marko, Mtakatifu Luka na Mtakatifu Mathayo,

**Somo la Februari 20, 2021 (Adar 8, 5781).**

## UTAKASO

**Somo Kuu: Waebrania 13: 9-21.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 17:17.**

1. Ni lazima mtu kwanza aamini Neno ili atakaswe? Yohana 17:19.
2. Je! Damu ya Yahshua inafanya nini? Heb. 13:21; 1 Yohana 1: 7.
3. Je! Ni sehemu gani nyingine kubwa ambayo Bwana Yahshua anahusika katika utakaso wetu? Heb. 10:14.
4. Je! Ni sehemu gani Roho Mtakatifu anahusika? Warumi 15:16; Matendo 1: 8.

**Maelezo**. - Kutakaswa ni kuwekwa wakfu kwa kusudi la utakatifu; Elohim anataka watumishi Wake wapate kuwekwa wakfu na kufanywa kamili.

5. Ni kazi gani muhimu inayoambatana na nguvu Yake ya kutia muhuri? Waefeso. 1:13, 14; 2 Wakor. 1:21, 22.
6. Je, Elohim anatuhitaji tuwe watakatifu? 2 Wakor. 7: 1; Wakol. 1:21, 22.
7. Kisha tunaingia katika hali gani ya utukufu? Waebr. 2:11.



4. Baada ya kujisalimisha kwa mwongozo wa Bwana, ni nini lazima kitekelezwe kikamilifu ili kupokea baraka ya Roho? Wagalatia 3:14.
5. Yahshua alitumia mfano gani kutofautisha kati ya uongo na ukweli? Mathayo 7: 15-20.
6. Ni tunda gani linalozaliwa katika maisha ya yule ambaye Roho anakaa ndani yake? Wagalatia 5:22, 23.
7. Je! Ni nini imesemwa kuhusu tunda lililotajwa kwanza? 1 Wakorintho 13:13. Wakolosai 3:14.
8. Je! Ni masisitizo gani ambayo mtume Paulo anaweka juu ya umuhimu wa kuwa na upendo? 1 Wakorintho 13: 1-3.
9. Upendo unadhihirishwa aje? Mistari 4-7.

**Maelezo**. Mtu anayesimama karibu na Masihi ni yule aliyekunywa sana roho ya kujitolea kikamilifu kama dhabibu kwa upendo - upendo ambao haujisifu, haujivuni - hautafuti mambo yake mwenyewe, haukasiriki kwa urahisi, haufikirii maovu, ni upendo uliomsukuma Bwana wetu kutoa yote, kuishi na kufanya kazi na kujitolea hata kwa kifo, kwa ajili ya kuwaokoa wanadamu.

10. Jinsi gani tunapata upendo huu mkuu? Warumi 5: 5.
11. Je! Upendo hufanya nini? Mithali 10:12; 1 Petro 4: 8.



anawezaje kubatizwa kwa ajili ya wafu kama ilivyoelezwa katika 1 Wakorintho 15:29?

8. Je, kufa kwa dhambi na vitu vyote katika maisha haya kutatufaidi katika maisha yajayo? Fikiria Warumi 6: 8-11.
9. Je! Ni ushauri gani wa ajabu Paulo anaoutoa katika Warumi 6:12, 13?
10. Kwa nini alitoa mawaidha haya? Warumi 6:14, 15.

******************************

**Somo la Machi 20, 2021 (Nisan 7, 5781).**

## MWILI WANGU NI CHAKULA CHA KWELI, NA DAMU YANGU NI KINYWAJI CHA KWELI

**Somo Kuu: Yohana 6: 22-71.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 6:54.**

1. Je, Yahshua alienda wapi baada ya kulisha watu elfu tano? Yohana 6: 24-25.
2. Ni kwa nini umati mkubwa ulimtafuta Yahshua? Yohana 6:26.
3. Yahshua aliwaambia nini kuhusu chakula? Alisema chakula hiki kinaweza kupatikana kutoka wapi? Yohana 6:27.
4. Je! Inaonekana kwamba umati huu ulifikiria kuwa ulikuwa na mkate huu kutoka Mbinguni? Jinsi gani Yahshua aliwajibu? Yohana 6: 31-35.



7. Yohana Mbatizaji alikuwa wapi wakati huu? Mathayo 3: 1-6.
8. Wakati watu walimwuliza Yohana Mbatizaji kama yeye ndiye Masihi, alijibu nini? Luka 3: 15-17; Yohana 1:19, 20.
9. Je! Ni pingamizi gani ambalo Yohana aliibua wakati Yahshua alikuja kwake kubatizwa? Je! Alihisi anastahili? Mathayo 3: 13, 14.
10. Yahshua alisisitiza aje umuhimu wa ubatizo? Mathayo 3:15.

**Maelezo**: Yahshua alikuwa mfano wetu kamili. Ingawa hakuwa na dhambi za kibinafsi za kuosha, alitimiza haki yote na kubeba dhambi zetu na maovu.

11. Baada ya kubatizwa kwake ni nini kilifanyika? Mathayo 3:16, 17.
12. Je! Sauti hii kutoka mbinguni ilisema kwamba Yahshua alikuwa mwana wa nani? Mathayo 3:17.
13. Baada ya Yahshua kubatizwa na kufunga kwa siku arobaini mchana na usiku, ni nani aliyemjia? Mathayo 4: 1.
14. Je! Shetani alipendekeza Yahshua afanye nini ili kudhibitisha kuwa yeye ni Mwana wa Elohim? Mathayo 4: 6, 7.
15. Baada ya haya, Shetani alimpa nini Yahshua ikiwa angemtii? Mathayo 4: 8, 9.

12. Je! Ni nini imesemwa juu ya fadhila zote za muumini? Wagalatia 5:23.

*******************************

**Somo la Februari 13, 2021 (Adar 1, 5781).**

## INJILI YA KWELI NI NURU NA NGUVU

**Somo Kuu: 1 Wakor. 1: 1-24.**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakor. 1:26.**

1. Je! Paulo alituambia nini juu ya nguvu ya injili? Warumi 1:16.
2. Wakati jina la Yakobo lilibadilishwa kuwa Israeli, ni nini imesemwa kuhusu yeye kuwa na nguvu, pamoja na Baba na pia na wanadamu? Mwanzo 32:28.
3. Je! Mwokozi wetu alikuwa na nguvu kiasi gani, katika kuleta wajumbe hawa wasioonekana kutoka mbinguni ili wamsaidie? Mat. 26:53, 54.
4. Tunapopokelewa katika kanisa la kweli, mwili wa Masihi, je! Tunahesabiwa pamoja, na pia kuwa washirika wa familia ya malaika? Waefeso 3: 14-16.
5. Je! Ni kweli kuwa malaika wa mbinguni ni ndugu zetu wenye imani moja na Baba mmoja? Ufu. 22: 8, 9.
6. Wakati hukumu za mwisho zitakuwa duniani, na mapigo saba ya mwisho kuwa juu ya ulimwengu



wote, ni nani atakayewakomboa washirika waaminifu wa familia hii moja? Zaburi 91:10, 11.

7. Je! Ni sababu gani iliyotolewa kwa malaika kuwakomboa washirika wa kweli wa familia hii takatifu wakati wa shida? Mstari wa 14; Danieli 12: 1.

**Maelezo**: Hizi ni sababu mbili zilizopeanwa hapa za ukombozi wakati huu wa shida. Moja ni "kuweka upendo wetu kwa Baba", ishara ambayo ni kushika amri zake (1 Yohana 5: 3), na nyingine ni kwa sababu tumelijua Jina Lake.

8. Je! Ni nini imesemwa juu ya familia iliyochaguliwa kuhusu nuru? Mat. 5: 14-16.
9. Katika wakati huu wa giza ni amri gani imetolewa kwetu kupeleka nuru ya kweli? Isaya 60: 1, 2.
10. Je! Familia hii, ambayo malaika ni sehemu yake, itajua kitu juu ya nyakati na majira tunayoishi, na wanajulikana kama watoto wa nuru? 1 The. 5: 1-6.
11. Kabla ya Yeye kuja kuhukumu dunia, ni sehemu gani hasa imetajwa ambayo taa hii itaangaza? Zaburi 50: 1-5.

*******************************



16. Mwishowe Yahshua alimwambia Shetani nini? Mathayo 4:10, 11.

*******************************

**Somo la Januari 16, 2021 (Shevat 3, 5781).**

## ULIMWENGUNI LAKINI SI WA ULIMWENGU

**Somo Kuu: Kumbukumbu la Torati 7: 1-11.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 17:15.**

1. Ni nani alikuwa mwanzilishi wa sehemu nzuri ya mataifa haya? 1 Mambo ya Nyakati 1: 13-16; Mwanzo 10:15. Kanaani alikuwa nani? Mwanzo 9:18.
2. Je! Mataifa haya yangeharibiwa na kufukuzwa mara moja? Kutoka 23: 27-33; Kumbukumbu la Torati 7:22.
3. Wafilisti waliendelea kwa muda mrefu kuwa maadui halisi wa Israeli. Je! Walikuwa na uhusiano wa karibu na makabila mengine? 1 Mambo ya Nyakati 1:12; Mwanzo 10: 7-11.
4. Je! Unalinganishaje Kumbukumbu la Torati 7: 2 na Kutoka 20:13?
5. Kwa nini Bwana hakutaka waolewe na mataifa haya ya kipagani? Kumbukumbu la Torati 7: 3-4. Lakini badala yake, wanapaswa kushughulika



**Somo la Machi 13, 2021 (Adar 29, 5781).**

## WAO WALIO WA MASIHI WAMESULUBISHA MWILI

**Somo Kuu: Warumi 6: 1-18.**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 5:24.**

1. Mwanzoni mwa Warumi 6, je! Paulo anaanzisha mada mpya, au anaendeleza mada ya sura iliyopita? Je! Unafikiri Paulo na wainjilisti wengine wanapaswa kudumu sana kuhusu somo hili?
2. Katika kuhubiri Injili ya Ufalme, je! Paulo alisisitiza juu ya mada hii, au zaidi juu ya neema, upendo, nk? Warumi 6:23.
3. Unafikiria ni nini maana ya kichwa cha somo hili? Tazama Wagalatia 5:24; Wakolosai 3: 5-9 na wengine wengi.
4. Kulingana na Warumi 6: 3, 4, ubatizo unaashiria nini?
5. Sasa, ikiwa tumekufa pamoja na Masihi katika kaburi lenye maji, je, tumewekwa huru kutoka kwa laana ya Adamu? Warumi 6: 6, 7.
6. Je! Unafikiri mateso ya mwili yaliyotajwa katika 1 Petro 4: 1, 2 yanahusu maumivu ya mwili? Eleza.
7. Injili ingewezaje kuhubiriwa kwa wafu kama ilivyoonyeshwa katika 1 Petro 4: 6 na mtu